# Pambazuko

*Ukweli Hauna Kutu*

Toleo Namba 008 — Jumatatu Agosti 29-Septemba 05, 2022




**YALIYOMO:**


**UK. 4** Tunatokaje kwenye mkwamo huu?

**UK.9** Tunafanya mzaha ajali za barabarani

**UK. 16** Ukiwa na miaka 35, jiulize mara mbili kupata mtoto


# Mmarekani ahamia Dar kwa kumhusudu Rais Magufuli

- *Asema aligoma kuabudu wazungu, matajiri*

**JISAJILI HAPA: Andika neno HABARI na tuma kwenye namba hii ya WhatsApp - 0744 768263 kupata gazeti bure**

# Nyamka katende haki, kabadilishe Magereza

RAIS Samia Suluhu Hassan amemteua Kaimu Kamishna wa Magereza Huduma za Urekebishaji, Mzee Nyamka kuwa Kamishna Jenerali wa Jeshi la Magereza (CGP). Anachukua nafasi iliyoachwa wazi na Meja Jenerali Suleiman Mzee ambaye hivi karibuni aliteuliwa kuwa Mkuu wa Mkoa wa Mara.

Kwanza gazeti la Pambazuko linampongeza kwa kuaminiwa na Amiri Jeshi Mkuu wa Vyombo vya Ulinzi na Usalama, Rais Samia kuliongoza jeshi hilo ambalo pia ni chombo kinachosimamia haki za binadamu.

Kazi kubwa ya jeshi hilo ni kuhifadhi watu ama wakiwa wamehukumiwa au wale wanaoendelea kusubiri hukumu zao kwenye vyombo vya sheria, hasa mahakama.

Katika kuwahifadhi, bado wanaotunzwa huko magereza ama mahabusu, wanaendelea kuwa binadamu, hivyo wanakuwa na haki zao za msingi kabisa. Kufungwa ama kuwa mahabusu, kamwe hakuondoi ubinadamu. Haki zake nyingi zinabaki palepale, isipokuwa anatengwa kulingana na hukumu aliyopewa na mahakama.

Sisi wa Pambazuko, tunapenda kuhimiza kwamba Afande Nyamka akaligeuze jeshi hilo ili lionekane linatenda haki kwa wote wanaokuwa chini ya jeshi hilo, na kamwe akaepuke kugeuka kuwa chimbo la mateso kwa kila anayehifadhiwa huko. Akifanya hivyo, atakuwa anajenga jeshi linaloheshimika.


Mara baada ya kuteuliwa, Nyamka alisikika akieleza kwamba anakwenda kuimarisha nidhamu, kufanya kazi kwa weledi, kujenga umoja na mshikamano kwa kuwafanya watumishi kuzungumza lugha moja.

Pia ameahidi kuendelea kuboresha programu za kurekebisha wafungwa, ili wakitoka, jamii iwaone wamebadilika na kwamba wakiwa ndani ya magereza, hakujifunza tabia mbaya zaidi, bali walirekebishwa na kuwa raia wema.

Nyamka amesema jeshi litatoa msukumo mkubwa katika jukumu la kuwalinda na kurekebisha tabia za wananchi waliovunja sheria, ili kuona wanabadilika na wawe tayari kujiunga na wenzao katika ujenzi wa shughuli za kimaendeleo wanapomaliza vifungo.

Ni vyema pia akatambua kwamba Magereza imezidiwa. Haina uwezo wa kuhifadhi wafungwa ama mahabusu wengi zaidi, hivyo aende akaone namna nzuri ya kushauri na hata kutenda, kupunguza mlundikano wa wafungwa, hasa kuhimiza kutumika kwa Bodi ya Parole na uamuzi wake kuheshimika.

Lakini mbali na Parole, akashauri vyema kuwaondoa wafungwa wanaoswekwa magereza kwa makosa madogo-madogo kama ya wizi wa kuku ili watumikie vifungo vya nje.




## Jisajili kupata Pambazuko bure

Ndugu msomaji wetu, jisajili kwa namba hii ya simu ya **WhatsApp: +255 744 768263** kwa kutuma neno **"HABARI"** kwa namba yako ya WhatsApp ili kupata Pambazuko kwenye WhatsApp yako.

Pia unaweza kujisajili kwa kutumia Email hii: pambazuko1@protonmail.com ili gazeti la Pambazuko likufikie kupitia email yako, andika neno **"HABARI"** na kutuma kwetu nawe utakuwa umejisajili.

## NUKUU



*"Umoja hautatufanya kuwa tajiri, lakini unaweza kuiepusha Afrika na watu wa Afrika kutoheshimiwa na kudhalilishwa na mataifa mengine, hasa tajiri" - kutoka katika hotuba aliyoitoa Accra, Ghana, Machi 6, 1997.*

# Tunatokaje kwenye mkwamo huu?

**Na Plato Hekimachius**

MARA baada ya kushika madaraka ya kuongoza nchi, Rais Samia Suluhu Hassan – kwa maneno yake aliyorudia mara kwa mara, kwamba "Tanzania ni yetu sote," alionekana kurudisha imani ya wananchi kwamba sasa nchi inakwenda mahali pazuri.

Kauli hiyo ya Rais Samia, iliondoa ukakasi wa "umimi" uliokumbatiwa mno na utawala uliopita, chini ya aliyekuwa mkuu wa nchi, Rais John Pombe Magufuli ambaye aliaminisha wananchi kwamba wenye hati miliki ya Tanzania ni viongozi wakuu, hasa yeye binafsi na pengine wachache ndani ya chama tawala, Chama Cha Mapinduzi (CCM).

Wakati ule, Rais Magufuli hakuamini kama nje ya CCM au yeye binafsi, kuna mawazo mazuri ya kuisukuma nchi mbele, wala kusaidia kuondoa changamoto za idadi kubwa ya wananchi – hasa hali ya ufukara inayoonekana kwa wananchi wengi, siyo wa vijijini tu, bali hata maeneo ya mijini.

Rais Magufuli aliamua kuwatosa mbali viongozi wa vyama vya siasa, wanazuoni wenye mawazo mbadala, viongozi wa dini, wanaharakati waliokuwa na mawazo yenye kujenga na hata wananchi wa kawaida. Hawa wote aliamini hawawezi kusaidia nchi.

Hata hivyo, hayo yaliyoonekana kwa Magufuli, bado yapo, licha ya kwamba Rais Samia amelegeza kidogo kamba ambayo ilitumiwa na mtangulizi wake "kuwamaliza" kabisa watu wenye itikadi, mitazamo na mawazo tofauti na yeye.

Rais Samia tofauti na "jeuri" ya mtangulizi wake, hivi sasa anaweza kuwaalika Ikulu watu wenye itikadi, mawazo na mitazamo tofauti na yeye ama chama chake na kufanya mazungumzo yanayohusu nchi. Hata hivyo, wengi hatuna uhakika kama mawazo ya hao "wageni waalikwa" anayatumia.

Kuwaalika Ikulu ni jambo jema, lakini ni jema zaidi ikiwa atatumia mawazo na



*Rais Samia Suluhu Hassan (Picha - Gazeti la Mwananchi).*

ushauri bora wa wananchi hao wenye mitazamo tofauti kujenga nchi, badala ya kukumbatia watu walewale miaka nenda rudi katika nafasi za uongozi. Huenda mawazo yaleyale ndiyo yamelifikisha taifa katika mkwamo.

Hata kuwalipa mali na stahiki wapinzani ambao waliumizwa na utawala uliopita, bado haitoshi, kuwaondoa magerezani na mahabusu bado pia hakutoshi, kuwaambia "rudini nyumbani tujenge nchi" nako hakutoshi na hata wachache kuwapa dhamana ndani ya serikali, hakutoshi aslani!

Pengine sasa ni wakati muafaka kwa Rais Samia kuita watu wenye mawazo mbadala kujadili juu ya masuala mbalimbali ya nchi.

Mfano anaweza kuanza kualika watu kadhaa na kujadili kuhusu tozo, kupanda kwa bei ya mafuta na masuala mengine ili kuzungumza namna ya kuondoka kwenye mkwamo. Na huko kuna uhakika kwamba atapata njia mbadala za kujikwamua.

***Inawezekana.***

# Tozo zafanya Watanzania 'kuandamana' mitandaoni

**Na Betty Massanja**

WATANZANIA hawana hulka ya kuandamana barabarani wanapopinga ama kuonyesha hisia zao wanapoguswa na jambo wanaloamini linawaumiza kama ilivyo kwa mataifa mengine.

Wao huumia kimyakimya – na mambo yanapowakaba sana, hulalamika chinichini – wakiwa wawili ama watatu. Hii siyo dalili ya woga, lakini ni tabia ya kuvumilia madhila iliyojengwa karne nyingi zilizopita.

Hata hivyo, kukua kwa teknolojia, kumewaibua Watanzania na sasa "wanaandamana" kupitia mitandao ya kijamii; hasa Twitter na Facebook na pia wanaonekana wakijazana kwenye Jamii Forums wakipaza vilio vyao.

Bila kujali jinsi, dini, itikadi zao za kisiasa wala taaluma zao, Watanzania wengi 'wanaandamana' kwa kupaza sauti juu ya kilio chao kwa madai ya kuumizwa na mafurushi ya tozo.

Wanalia kwa kuwepo ongezeko la kodi (maarufu -Tozo Umiza) karibu katika kila bidhaa na huduma, hivyo kufanya maisha yao kuwa magumu kila uchao.

Hali hii pamoja na kuelezwa na serikali kwamba inatokana na vita vya Russia dhidi ya Ukraine na maelezo mengine, bado haitoshi kuwepo kwa maumivu hayo katika kila eneo.

Pengine wapo wanaodai ongezeko hilo linakomazwa na kuwepo kwa 'mchwa' wanaotafuna fedha za kodi za wananchi kwa manufaa binafsi na familia zao. Fedha ambazo zilizopaswa kuwa za Watanzania wote.

Watanzania wengi wanaeleza kwamba wezi wa mali za umma bado wapo, na huenda wameongezeka mno kwa kuwepo kauli iliyowahi kutolewa na serikali kwamba – "najua mnakula kwa urefu wa kamba zenu, lakini msivimbiwe".



*Waziri wa Fedha, Dkt. Mwigulu Nchemba*

Mwenendo huo wa baadhi ya wafanyakazi kutumbua mabilioni ya fedha kwa "urefu wa kamba, uroho na ubinafsi," kunakomaza mno mzigo huo mzito wa tozo na kushindwa kubebeka.

Kwa kauli hii, hata jitihada za kufichua mchwa hao kupitia Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (MMHS) au CAG, bado hakuonekani kusaidia. Serikali haichukui hatua kwa wanaopatikana na matumizi mabaya ya fedha, wizi na hata rushwa.

Ni vyema sasa serikali ilete orodha ya wabadhirifu wote waliowajibishwa na kiasi cha fedha walizozirejesha au kufilisiwa mali zao kwa manufaa ya umma kufuatia uchunguzi wa CAG.

Watanzania wanatamani kushuhudia vinara wa ubadhirifu wa fedha za umma wanarejesha mali za umma walizojilimbikizia kwa kuzipora ili zitumike kuleta maendeleo.

Kwani kwa kufanya hivyo, kunaweza kuwa tiba; ya kupunguza kama siyo kukomesha kabisa tabia ya wizi wa fedha za umma.

# Nyuklia yaamsha matajiri



*Rais wa Marekani, Joe Biden (Picha na Financial Express)*

HOFU ya kuanza kutumika kwa mabomu ya nyuklia katika vita vya Russia na Ukraine, imeongezeka baada ya kuwepo fununu ya kulipuliwa.

Russia kama ilivyo kwa Ukraine, ina vituo vya mabomu hatari ya nyuklia. Kila taifa limekuwa likisikika kueleza kwamba, endapo italazimika, basi litafanya kila linalowezekana kulipua vituo hivyo.

Mataifa tajiri ya magharibi yamesisitiza kuhusu haja ya "kuimarishwa kwa usalama" wa vituo vya nyuklia ili visilipuliwe na kuleta madhara makubwa.

Uingereza, Ufaransa, Ujerumani na Marekani zimesisitiza kuwa kushambuliwa kwa vituo hivyo "kunahatarisha usalama wa dunia nzima."

***Reuters (Kyiv, Ukraine)***

## Serikali kuwajibika

WAZIRI Mkuu wa Somalia, Hamza Abdi Barre ameahidi kuwajibika kwa serikali yake kufuatia mashambulizi ya magaidi wa Al-Shabaab yaliyoua watu 21 mjini Mogadishu, Ethiopia.

Hata hivyo, hakueleza serikali yake itawajibika namna gani.

Kiongozi huyo amewataka raia wa Somalia kuungana dhidi ya wanamgambo hao ambao wamekuwa wakiendeleza mashambulio nchini humo kwa miaka 15 iliyopita.

Magaidi hao walishambulia mgahawa wa Hayat katikati wa jiji la Mogadishu ambapo pia watu 117 walijeruhiwa katika shambulio hilo.

Maofisa wa serikali walisema zaidi ya watu 100, wakiwemo wanawake na watoto, waliokolewa baada ya magaidi hao kuwateka wateja waliokuwa ndani ya hoteli kwa saa 30.

Shambulio hilo ndilo baya zaidi kutokea nchini Somalia tangu Rais Hassan Sheikh Mohamud kuchaguliwa Mei 2022.

***-Mashirika (Mogadishu, Somalia)***

## Njaa kali tishio Afrika

NCHI za Pembe ya Afrika inayojumuisha Kenya, Ethiopia na Somalia zitaendelea kukabiliana na njaa na huenda vifo vikaongezeka endapo msaada wa haraka hautapatikana, utafiti wabaini.

Ripoti ya Shirika la Hali ya Hewa Duniani (WMO) iliyotolewa wiki iliyopita inaeleza kwamba uhaba wa chakula utaendelea kushuhudiwa katika nchi hizo kufuatia ukame unaosababishwa na mabadiliko ya tabianchi.

Ripoti hiyo inaonyesha kuwa nchi hizo za Pembe ya Afrika zimeingia katika msimu wa tano wa kuwa na mvua kidogo.

***- BBC (Geneva, Uswisi)***

# 'Matundu' ya IEBC kuonekana

**Na Midlajy Maez**

NILIPATA wasaa wa kufuatilia mubashara tukio la kuzinduliwa rasmi kwa matumizi ya Katiba mpya nchini Kenya Agosti 27, 2010 kupitia televisheni.

Rais wa nchi hiyo kwa wakati huo, Mwai Kibaki, mbele ya idadi kubwa ya viongozi wa mataifa mengine na mabalozi, alisema kuanza kutumika kwa katiba hiyo mpya ni kuridhia matakwa ya Wakenya asilimia 67 walioridhia kuwepo kwa katiba hiyo mpya.

Makali na uzuri wa katiba hiyo yalianza kuonekana mwaka 2017 baada ya mahakama 'kuharamisha' ushindi wa Uhuru Kenyatta na kulazimisha kurejewa kwa uchaguzi huo. Hii ilitokana na sababu ya kuwepo kifungu kinachoruhusu matokeo ya urais kupingwa mahakamani.


Kile kilikuwa kipimo cha nguvu za katiba mpya na sasa nguvu hiyo imeonekana katika matokeo ya uchaguzi mkuu wa nchi hiyo uliofanyika Agosti 9, 2022.

Uchaguzi wa mwaka huu chini ya Tume Huru ya Uchaguzi na Mipaka ya Kenya (IEBC) yenye mfumo ulioboreshwa ilikuwa mtihani mwingine kwa Katiba mpya ya Kenya! Baada ya kumtangaza mgombea wa Kenya Kwanza, Samwel Ruto kuwa mshindi, akimpita mpinzani wake mkubwa, Raila Odinga wa Azimio la Umoja.

Hata hivyo, Raila amekwenda mahakama ya juu kabisa ya nchi hiyo kupinga Ruto kutangazwa mshindi wa urais kwa madai kadhaa, kubwa ikiwa ni "wizi wa kura" na kuingiliwa kwa mifumo ya kukusanya taarifa ya tume hiyo.

Madai ya Raila ni mtihani kwa mfumo ulioboreshwa wa IEBC na hasa uimara wa Katiba mpya Kenya. Je, mfumo huo uko sawasawa au umeanza kuchacha au tayari wajanja wameshaingilia tume hiyo?

Kama ilivyokuwa kwa Uhuru, ni matumaini kwamba mahakama ya juu itatenda haki na kila mgombea – Ruto na



*Raila Odinga*

Raila wataheshimu ili kulinda amani ya Kenya na maendeleo yake.

Endapo mmoja wao atadharau uamuzi wa mahakama hiyo, upo uwezekano mkubwa wa kuzuka kwa vurugu na machafuko ambayo, siyo tu kwamba yataumiza wananchi na hata vifo, bali yatavuruga taswira na mchakato mzima wa IEBC na watendaji wake- hasa mwenyekiti Wafula Chebukati.

Hatua ya Raila kwenda mahakamani kupinga Ruto kutangazwa mshindi, ni haki yake na wala asionekane ni king'ang'anizi wa madaraka. Anatimiza wajibu wake akiwa raia wa Kenya.

Raila kwenda mahakamani pia ni muhimu zaidi kutoa mwanya wa kuona wapi kuna "matundu" ndani ya IEBC ili iwe imara zaidi kusimamia uchaguzi nchini humo.

Wanaobeza hatua ya Raila hawana nia njema na mustakabali wa nchi ya Kenya na nchi zingine za Afrika ambazo zinapaswa kubeba mazuri ya kuwepo kwa Katiba mpya.

***Mwandishi ni mjumbe wa Jukwaa la Wahariri Tanzania (TEF).***

# Ubunifu kama uumbaji

**Na Askofu Dkt. Stephen Munga**



TULIANGALIA kwa kifupi juu ya watu ni nani. Lengo kubwa lilikuwa kujua sifa za msingi za mtu ambaye yeye ndiye mbunifu na mtengenezaji wa siasa (safi); pia mchezaji katika timu ya uongozi (bora).

Katika makala yale nilimtengeneza mtu huyo kimaadili. Nilifanya hivyo kwa makusudi ya kutoa picha ya msingi ya mtu ambaye ni muwajibikaji. Mtu huyo anao uwezo wa kuona mambo katika uhalisia wake; anaweza kubadilisha mtazamo bila kuharibiwa mwenyewe; anaweza kubadilisha mambo kwa utambuzi wa kujua yaliyo mema na yaliyo mabaya kwa ajili yake na kwa ajili ya wengine.

Mtu huyo ni bora na ambaye ni kielelezo cha wema na ambaye ni kipimo cha juu cha watu wengine kujilinganishia. Anaheshimu na ana imani na watu wengine na pia anaheshimika na kuaminika kwa watu wengine.

Sasa nijenge daraja la kumuingiza katika wajibu wa kubuni na kuumba fikra bora za siasa. Ubunifu (creativity) ni kipawa na fani. Maana yake hapa ni kwamba anaweza kuwa mbunifu ama kwa kipawa cha kuzaliwa au kwa kutaalumishwa.

Ubunifu ni sanaa ambapo mtu huumba jambo kulingana na upeo wa mtazamo wa nafsi na akili zake. Ubunifu ni wazo changamano linalodhihirisha uwezo na upeo wa mtu wa kuumba kitu kipya. Ni mfano wa kuimwaga nguvu ya upenzi na nafsi katika kutokelezesha kitu kile ambacho akili inapambana kukifikia katika upeo wa juu wa ubora.

Sifa za mtu yule niliyemtengeneza katika makala zilizotangulia na jinsi alivyokua kijamii; maendeleo kimakuzi na kielimu; na uzoefu aliopata katika maisha, ambapo hayo humjengea tabia iliyo kichocheo kwa ubunifu.

Hoja wakati ule ilikuwa kwamba uumbaji ni sifa ya Mungu pekee ambapo huchukua sura ya kuasilisha uwepo wa vitu kutoka ukiwa na utupu (creation from nothing = creatio ex nihilo). Ambapo aliyeumba (Mungu) ni wa milele lakini kilichoumbwa siyo cha milele.

Kwa mantiki hiyo, aliyeumbwa hawezi kuwa muumbaji. Kwa hiyo wanadamu wajapokuwa na akili kubwa kiasi gani, lakini kamwe hawawezi kuwa waumbaji. Tukitembea katika uelewa huo natumia ubunifu kama uumbaji kwa mtazamo wa kiuwakili (stewardship).

Hitimisho la uumbaji wa Mungu lilikuja na utume wa Mungu kwa watu wa kutunza uumbaji huo. Kwa hiyo, ndani ya mtu kuna nguvu ile ya kuendeleza uumbaji ili kuufanya ulimwengu kuwa mahali bora zaidi.

Uasi na anguko la dhambi viliasilisha nguvu iliyo kinyume na uumbaji yaani uharibifu. Kwa hiyo tunafeli katika utunzaji wa uumbaji (kama uharibifu wa mazingira) kwa sababu ipo nguvu hasi ya uharibifu ndani ya watu. Hata hivyo, hapo naongelea nguvu chanya ya mtazamo wa kiuumbaji iliyomo ndani ya kila aliyeumbwa.

Wazo hilo la uwakili ndio msingi wa mimi kutumia ubunifu kama namna ya kuumba. Siyo kuumba kitu kutoka utupu na ukiwa, bali kuumba kitu kipya kutoka vilivyopo. Kwa hiyo mtu yule wa kutengeneza siasa safi ni muhimu awe mbunifu katika kuumba siasa safi zenye manufaa kwa jamii.

## Mezani kwa Chahali



**Na Evarist Chahali**
evarist@chahali.com

# Tunafanya mzaha ajali za barabarani

KUNA matukio matatu yaliyojiri wiki iliyopita ambayo yote yanahusiana na usalama barabarani; moja la kimataifa, mawili ni ya huko Tanzania.

Katika tukio la kimataifa, Paul Pelosi ambaye ni mume wa mwanasiasa maarufu nchini Marekani, Spika wa Baraza la Wawakilishi (Congress), Nancy Pelosi, alihukumiwa kifungo cha siku tano jela kwa kosa la kuendesha gari akiwa amelewa.

Kwa mujibu wa Katiba ya Marekani, Spika ni nafasi ya pili baada ya Makamu wa Rais kuweza kurithi urais endapo lolote litamkumba Rais wa nchi hiyo. Kwa kifupi, ni moja ya nyadhifa za juu kabisa nchini humo. Na kufungwa kwa mumewe, ingawa kwa siku chache siyo jambo dogo.

Katika matukio mawili yaliyojiri huko Tanzania; la kwanza ni kauli ya Kamanda wa Kikosi cha Usalama Barabarani, Wilbrod Mtafungwa (pichani) kwamba "ajali hizi ni kazi ya shetani."

Katika habari husika, ilielezwa kuwa Watanzania zaidi ya 50 wamepoteza maisha ndani ya mwezi mmoja.

Tukio la pili ni "hukumu ya mzaha" aliyopewa mtoto wa waziri mmoja ambaye licha ya kusababisha ajali, aliendesha gari akiwa amelewa na pia alitukana askari polisi na raia wasio na hatia.

Baada ya kukiri makosa, alihukumiwa kulipa sh. 250,000 sambamba na leseni yake kufungiwa miezi sita.

Kwa wenzetu huku nchi za magharibi, kosa la kuendesha gari ukiwa umelewa linachukuliwa kwa uzito mkubwa kwa sababu iliyo wazi; dereva aliyetumia kilevi ana uwezekano mkubwa wa kusababisha ajali.

Ndio maana licha ya kuwa mume wa Spika wa Congress ya Marekani, Paul Pelosi alitupwa jela kwa siku tano.



*Kamanda Mutafungwa*

Kwa upande wetu, bado kuna mzaha mkubwa katika kuhakikisha usalama wa barabarani, na yayumkinika kuhitimisha kuwa mzaha huo una mchango mkubwa katika wimbi la ajali zinazogharimu maisha.

Kauli ya afande Mtafungwa kwamba wimbi la ajali ni kazi ya shetani ni 'fyongo.' Chanzo kikuu cha ajali ni rushwa, ambayo huwafanya baadhi ya askari wa barabarani (trafiki) wasio waadilifu, kufumbia macho makosa ya madereva na/au vyombo vyao vya usafiri.

Kwa upande mwingine, "adhabu ya mzaha" aliyopewa mtoto wa waziri inaweza kuwahamasisha "watoto wa vigogo" kutochelea kuendesha magari wakiwa wamelewa.

Mwisho, serikali na Jeshi la Polisi zinapaswa kutupia jicho kasumba ya rushwa miongoni mwa trafiki na kuidhibiti.

# Mmarekani ahamia Dar

**Na Mwandishi Wetu**

MWANAZUONI, mtafiti na mwandishi wa vitabu kutoka Marekani, Bamidele Best, Julai, 2020 alikata shauri kundoka nchini kwake na kuhamia Afrika. Nchi aliyoichagua ni Tanzania.

Sababu kubwa ya kuchagua kuanza maisha mapya yeye na familia yake nchini Tanzania ni "kumkubali" na kuamini maono ya aliyekuwa kiongozi wa awamu ya tano wa nchi hiyo, John Pombe Magufuli.

Akizungumza na gazeti la Pambazuko, Bamidele anaeleza sababu zingine za kuamua kuja Tanzania, na kuchagua kuishi Jiji la Dar es Saaam, ni ukarimu wa watu wake, chakula cha asili na pia hali ya hewa.

"Baada ya kutambua kwamba asili ya binadamu ni Afrika, nikaendelea kujiuliza, kwanini tuendelee kuishi utumwani huku Marekani? Kwanini tusirudi kwenye mizizi ya mabibi na mababu zetu? Kwanini tuendelee kuwa ndani ya utumwa hapa Marekani? Ndipo mimi na mke wangu, Naila na kijana wetu tukamua kuja Afrika kwa mara ya kwanza na kuishi moja kwa moja," anaongeza Bamidele.

Akiwa mtumishi wa Shirika la Ndege la Marekani la Delta, akiishi Atlanta, aliacha mshahara na makazi yake na kuanza safari ya muda wa saa 22 na dakika 50 kuja Dar es Salaam, Tanzania. Safari ya kilomita 14, 491 angani.

Bamidele anaeleza kwamba pamoja na lengo lilikuwa kwenda Ghana, ambako kuna jamii kubwa ya Wamarekani weusi walioamua kurudi Afrika, lakini baadaye familia yake iliamua kuelekea Tanzania.

**Kwanini Magufuli?**

Bamidele anaeleza kwamba misimamo na kile anachokiita maono ya Rais Magufuli, yalimpa msukumo wa kuja Tanzania, kwani hakuamini kusikia kiongozi huyo akiwagomea wazungu na matajiri.

"Mara zote tangu nakua, nasoma



*Bamidele akiwa na familia yake, mkewe - Naila na kijana wao wa kwanza, Mikey*

ama kuona kwenye televisheni za Marekani namna viongozi wa Afrika wanavyowapapatikia Wazungu, hasa kutoka nchi tajiri kama Marekani, Ufaransa, Uingereza na Canada, lakini hali hiyo ni tofauti kabisa kwa Magufuli, yeye alikuwa na misimamo yake, hakuwaabudu kamwe," anasema Mmarekani huyo.

Anatoa mfano mmoja uliomfurahisha katika misimamo ya Rais Magufuli kuwa ni suala la janga la Covid-19, akielezea kwamba kiongozi huyo wa Tanzania alijua ujanja wa nchi na watu matajiri duniani kuhusu ugonjwa huo, hivyo aliwagomea na wakamchukia.

Mbali na msimamo huo, Bamidele anataja sababu zingine za kumkubali Magufuli kuwa ni kudhibiti rushwa, kuongeza utendaji na uwajibikaji wa watumishi wa umma na kutokumbatia watu wenye fedha, tofauti na viongozi wengi wa Afrika.

Rais Magufuli alifariki dunia Machi 17, mwaka jana- 2021.

**Kuishi Marekani ni kama jela**

Bamidele ambaye anaamini katika Uafrika kwa kuendesha maisha yake ya kila siku pamoja na familia, anadai kukaa Marekani, bila kujali ni mji gani, ni sawa na kuwa kifungoni, kwamba maisha ni magumu na yaliyojaa hofu.

"Huku watu wanaona maisha ya

# Mmarekani ahamia Dar

Marekani kuwa ni bora zaidi, lakini hakuna uhuru, kuna utumwa, vijana wengi wanadanganywa na sanaa wanazoziona kwenye televisheni za huko, lakini kuna mateso makubwa sana," anaongeza.

Katika website yake; www.witnessourdivine.com, Bamidele anaandika kwamba; "ninashukuru Mungu kwa kuondoka jela, bada ya miaka mingi ya mateso, nikiwa Marekani."

Anasema kwamba malezi ya watoto ukiwa Marekani ni mabaya zaidi kuliko sehemu nyingine yoyote duniani kwani vijana hubeba tabia za hovyo, ikiwamo kujifunza kuua, kuvuta bangi na kuikataaelimu.

**Wamarekani wengine wanamuonaje?**

Bamidele anasema kuwa walipoamua kurejea Afrika na hasa Tanzania, Wamarekani wengi marafiki zetu walidai kwamba yeye na familia yake wamechanganyikiwa na kwamba lazima watarejea Marekani.

"Hata hivyo, wengi sasa wameanza kuona namna tunavyopata maisha mazuri yasiyokuwa na hofu yoyote kama wao, na wanaomba kuja kuishi Tanzania, mimi nawakaribisha na muda siyo mrefu, tutakuwepo Wamarekani wengi zaidi Tanzania tulioamua kurudi kwenye mizizi yetu," anaongeza.

Anasema hofu ya Wamarekani wengi kuja kuanza maisha Afrika, imejengwa na vyombo vya habari ambavyo kila mara huonyesha Afrika kuwa ni eneo la machafuko, vita na magonjwa.

**Sasa anafanya nini kupata kipato?**

Anaeleza kwamba vyanzo vyake vya mapato vinatoka kwenye kuuza vitabu, kufundisha watu wengine juu ya Uafrika na mifumo yake kwa njia ya mtandao na pia mke wake ni mhariri wa video.

**Changamoto anazopata**

Bamidele anaeleza kwamba tangu afike na kuanza maisha Dar es Salaam, changamoto kubwa ilikuwa lugha; yeye anazungumza Kiingereza, lakini watu wanaomzunguka wanazungumza Kiswahili, hivyo alipata shida kuelewana nao.



*Kitabu alichoandika Bamidele*

Hata hivyo, kadri muda ulivyokuwa ukisonga, aliamua kuwa mwalimu wa kujitolea kuwafundisha Kiingereza huku wao wakimfundisha Kiswahili, na sasa kidogo anamudu kuwasiliana bila kikwazo.

Anaeleza kwamba kwa sasa kujifunza Kiswahili ni kipaumbele kwake na familia na kwamba kijana wake anaelewa zaidi lugha hiyo kuliko yeye na amekuwa msaada wa kumfundisha zaidi.

"Muda mfupi ujao, hapa nyumbani tutaacha kabisa kuzungumza Kiingereza, itakuwa ni Kiswahili tu kwa "kwenda mbele."

Hivi sasa Bamidele, baba wa watoto wawili, mmoja akimpatia Tanzania, anayeitwa Jahi, ana mpango wa kuanzisha taasisi ambayo kazi yake kubwa ni kuhimiza Wamarekani kuja kuishi na kufanya kazi Tanzania na kuondoka Marekani ambako anaendelea kusisitiza ni "kifungoni."

# Hivi Tanzania inakwama wapi kukabili ufukara?

**Na Godwin Chilewa, Texas, Marekani**

ZIPO dalili kedekede zinazoonyesha kuwa Tanzania haijajipanga vyema kukabili dharura au majanga ya kidunia, mojawapo ya dalili hizo ni kutokuwepo kwa akiba kubwa ya mafuta ya kuendesha mitambo.

Wakati nchi zingine zikiwa na akiba ya mafuta kwa miaka miwili – wakati wote, Tanzania inaeleza kuwa na akiba ya miezi miwili tu ya nishati hiyo muhimu.

Nchi kuwa na akiba kidogo ya mafuta, ni hatari sana, kwani kunapotokea majanga ya asili; mafuriko, kimbunga, matetemeko, au hata yale yanayosababishwa na binadamu - kama vile vita, maendeleo wa nchi huwa shakani. Mafuta yakikosekana, hakuna kinachoendelea!

Ni muda muafaka sasa kwa Tanzania kupanga mipango ya kuwa na akiba ya mafuta kwa angalau mwaka mmoja, ili kuhakikisha kuwa kwa kipindi hicho, endapo kutatokea lolote, uchumi wa nchi hautaporomoka na maisha ya watu wake yataendelea.

Mbali na suala la kuhifadhi mafuta ya kutosha ili kujilinda na kuporomoka kwa uchumi, ni wakati muafaka sasa kwa serikali anayoongoza Rais Samia Suluhu Hassan, kubadili mtazamo na mfumo wa kupambana na ufukara wa wananchi.

Rais Samia apangue mifumo aliyoikuta na ajenge yake ambayo siyo tu itaacha alama ya uongozi wake, bali itainua, kuimarisha na kuboresha maisha ya watu anaowaongoza.

Awekeze zaidi mitaji, utaalamu na fursa kwenye miradi ya uzalishaji mali inayosaidia wananchi kuinua kipato chao.

Hivi sasa bado serikali inasuasua kuwa na mikakati ya uwekezaji mkubwa katika kilimo cha mboga, matunda, mazao ya nafaka, na hata mazao ya biashara japokuwa ardhi yenye rutuba iko bwelele.



*Hali ya umasikini uliokithiri (Picha ya Dreamstime.com)*

Hili pengine linatokana na mtazamo uliopo hivi sasa kuwa serikali kazi yake ni kukusanya kodi tu, na siyo kujihusisha moja kwa moja na shughuli za kuwekeza katika njia kuu za kuimarisha uchumi.

Hata hivyo, ukiziangalia kwa makini nchi nyingi zilizoendelea, utaona kuwa maendeleo ya kilimo, biashara na viwanda katika nchi hizo yamechangiwa kwa kiasi kikubwa na mikakati ya serikali kuwawezesha wahusika kwa hali na mali.

Hebu jiulize kwa nini serikali haiweki kiwanda cha kusindika vinywaji vitokanavyo na mabibo mikoa ya kusini, au sehemu nyingine kunakolimwa zao hilo?

Kwa nini tunashindwa kuwa wauzaji wakubwa wa maparachichi duniani wakati kule Mbeya matunda hayo yanaoza tu? Kwa nini tunaagiza mafuta ya kula nje wakati alizeti, michikichi, minazi, karanga, maparachichi na ufuta vimejazana nchini?

Napenda kusisitiza haja ya viongozi wetu kuwa na maono mapya katika kuliendeleza taifa. Ni ukweli usiopingika kuwa serikali ya awamu iliyopo inajitahidi kupambana ili kubadilisha hali ya maisha ya wananchi, hata hivyo mapambano hayo hayawezi kuwa rahisi, wala kutufikisha mbali kama fikra na mtazamo wa walio wengi utabaki kama mazoea yaliyopita na kuwa na maono ya ‘tozo–tozo’ tu.

# Soko la fedha Somaliland

**H**ILI ni soko la kubadilisha fedha la mji wa Hargeisa ulioko Somaliland. Ni eneo maarufu kwa wenyeji na wageni wanaotaka kubadilisha fedha kwa ajili ya matumizi ya ndani ya nchi hiyo au wale wanaosafiri nje.





**Fedha ya nchi hiyo inaitwa Shilingi.**

Jana Shilingi 1,000 ya Tanzania ilikuwa ikibadilishwa kwa Shilingi 243 za Somaliland. Dola 1 ya Marekani ni sawa na Shilingi 571 za Somaliland. (Picha hizi zimetoka vyanzo mbalimbali vya mtandao).



# Tutakumbuka Daima...



*Kwamba Mwalimu Julius Kambarage Nyerere, alikuwa mpenzi wa kuendesha baiskeli kila alipopata wasaa wa kufanya hivyo. Mwalimu aliamini kwamba baiskeli pamoja na kwamba ni usafiri, lakini ni chombo muhimu cha kufanya mazoezi. (Picha kutoka Maktaba ya Pambazuko*

# Ngeli za Nomino




**Na Dkt. Michael Mashauri**

KISWAHILI ni miongoni mwa lugha zinazokua kwa kasi kubwa kila siku duniani. Vyuo vikuu nje ya Afrika, vimeanza kufunza lugha hiyo adhimu. Kutokana na umuhimu wake, Pambazuko limeamua – kila wiki, kuwa njia ya kufundisha Kiswahili bure kwa yeyote anayependa.

Leo tutaendelea na somo la ngeli ambalo hujumuisha majina ya lugha na vitu vingine mbalimbali visivyo na uhai vinavyoanza viambishi **KI-** au **CH-** katika umoja na **VI-** au **VY-** katika wingi. (This noun class includes names of languages and other inanimate things whose names begin with **KI-** or **CH-** in singular and **VI-** or **VY-** in plural. Examples:

| Prefixes | | Class | Examples | | English translation |
|---|---|---|---|---|---|
| Singular | Plural | | Singular | Plural | |
| ki- | vi- | KI-/VI- | kiti | viti | chair/chairs |
| ki- | vi- | | kitabu | vitabu | book/books |
| ki- | vi- | | Kiswahili | - | Swahili language |
| ch- | vy- | | chakula | vyakula | food/foods |
| ch- | vy- | | chumba | vyumba | room/rooms |
| ch- | vy- | | chandarua | vyandarua | mosquito net/ mosquito nets |

Kuna majina mengine ya viumbe hai ambayo huanza na KI- katika umoja na **VI-** katika wingi lakini hayaingii katika ngeli hii ila **M/WA** (There are some names for animate things that begin with **KI-** in singular and VI- in plural but do not fall under this noun class. They are in **M/WA).** Examples:

kiongozi – viongozi (leader/leaders)
kipofu – vipofu (blind/blind)
Other names like chai (tea), chupa (bottle) are in **N/N** noun class.

**N/N noun class**

Ngeli hii hujumuisha majina ya vitu mbalimbali visivyo na uhai ambayo hayana viambishi vya umoja na wingi (This nouns class consist of various names of inanimate things whose structures do not have singular or plural prefixes) Examples:

| Prefixes | | Class | Examples | | English translation |
|---|---|---|---|---|---|
| Singular | Plural | | Singular | Plural | |
| N- | N- | N/N | nguo | nguo | clothes |
| N- | N- | | ndizi | ndizi | banana/s |
| N- | N- | | saa | Saa | watche/s |
| N- | N- | | meza | meza | table/s |
| N- | N- | | nyumba | nyumba | house/s |

Majina ya wanyama hayana umoja na wingi lakini yanajumuishwa katika ngeli ya M/WA kwa kuwa ni viumbe hai (Animal names have no singular and plural prefixes but they are included in the **(M/WA)** noun class since animals are animate). Examples: simba (lion/s), twiga (giraffe/s), ndege (bird/s).

***Mwandishi wa Darasa la Kiswahili ni Mhadhiri wa Chuo Kikuu cha DSM***

# Ukiwa na miaka 35, jiulize mara mbili kupata mtoto



*Mbegu za kiume (Picha ya MH)*

**MARA** nyingi imezoeleka kwamba wanawake, wanaofikisha miaka 35 na zaidi, ndiyo wenye kukumbwa na madhila ya kupata mtoto, lakini kumbe hata wanaume.

Wanawake, kwa miaka nenda rudi, wamekuwa wakibeba lawama kutoka kwenye jamii wanazoishi, kila wanapochelewa ama kupata mtoto mwenye changamoto za afya kama ulemavu. Sababu nyingi hutolewa; za kitaalamu na zingine za "kienyeji."

Hata hivyo, sayansi sasa imebaini kuwa wanaume wanaoamua kuwa wazazi – wakiwa na miaka 35 na kuendelea, wanakabiliwa na hatari ya kupata watoto wanaozaliwa kabla ya muda au kuwa na ulemavu- wa viungo au hata akili.

Inaelezwa kitaalamu kwamba kila mwaka unaokwenda, mbegu za uzazi za kiume hupungua kwa kiasi kikubwa kwa wingi na ubora wake, jambo linaloweza kuhatarisha uwezo wa kuendeleza kizazi.

Utafiti uliofanywa miaka mingi na sasa kuthibitika, unaweka wazi kwamba wanaume wenye umri huo na zaidi, wanapaswa kupata ushauri wa kitabibu kutoka kwa madaktari bingwa ili kufahamu njia nzuri za kupata mtoto mwenye siha njema.

Hivi karibuni, utafiti uliofanywa na Kitivo cha Tiba cha Chuo Kikuu cha Stanford, Marekani, ambacho kilitathmini kumbukumbu za mbegu za uzazi zaidi ya milioni 40, umebaini kwamba kadri mwanaume anavyoendelea kukua, ndivyo athari za kupata mtoto mlemavu zinaongezeka.

Watoto wanaopatikana wanaweza kuwa na changamoto kadhaa, kubwa ikiwa ni; kuzaliwa wakiwa na uzito mdogo, magonjwa ya akili, kifafa, mfumo wa kupumua na mengineyo.

Katika hitimisho, utafiti huo unabainisha kuwa, kwa kila miaka 10 ya ongezeko la umri wa mwanaume, kuna asilimia 21 ya fursa ya ziada kwamba mtoto anayezaliwa atakuwa na changamoto za afya.

Hata hivyo, pamoja na hali hii, inaelezwa pia kuwa kupungua kwa ubora wa mbegu za uzazi za kiume, huchangiwa na uimara wa mfumo wa seli za uzazi na afya ya mama anayebeba.

***Sehemu kubwa ya makala haya yaliyohaririwa, yametoka BBC***

# Mrema: Ofisa kipenyo aliyewatisha wakubwa

**Na Simon Mkina**



ALIWAHI kuwa mkulima kijijini kwao, akawa mwalimu wa shule za msingi kadhaa na baadaye akapata ajira ndani ya Idara ya Usalama wa Taifa - akawa ofisa kipenyo.

Baadaye akaingia kwenye siasa. Akaanza kwa kugombea ubunge wa Jimbo la Moshi Vijijini, ukashinda na kuwa mwakilishi wa wananchi kwa vipindi viwili (miaka 10; 1985 – 1995).

Augostino Lyatonga Mrema, ambaye umahiri wake akiwa bungeni; wa kufuatilia kwa makini hoja za serikali, kuuliza maswali na kuchangia mijadala – pamoja na mambo mengine, akakupa fursa ya kuwa Waziri wa Mambo ya Ndani wa Tanzania.

Utendaji wake Mrema, akiwa waziri; bila kujali kama ulikuwa unafuata sheria na hata haki katika kutekeleza majukumu, alizoa sifa kedekede.

Katika utendaji, hakuogopa wadhifa, udugu na hata urafiki, alichukua hatua kwa kuagiza Jeshi la Polisi kufanya kazi yake. Aliwasweka ndani jamaa wa rafiki na hata ndugu na alikuwa akisisitiza kwa kusema; "uwaziri wangu hauna udugu."

Ni kutokana na tabia hiyo, alikwaruzana na baadhi ya mawaziri wenzake, wakubwa wa majeshi na viongozi wengine waliompachika kilemba cha kuwa ni "kimbelembele" kwa Rais Ali Hassan Mwinyi.

Rais Mwinyi, mtu muungwana sana, asiyependa makuu, akaona heri amuongezee nguvu ili afanye kazi yake vyema zaidi na aogopeke. Akampa cheo kisichokuwamo ndani ya Katiba; Mrema akawa Naibu Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Kwa tabia yake, cheo hicho kikamkupa "spidi" zaidi akawa 'anafyatuka.' Akiagiza watu kukamatwa, akimuru kuwekwa korokoroni na hata akaanzisha utaratibu wa kuelekeza baadhi ya wafanyabiashara – hasa wenye asili ya Asia walioko Dar es Salaam na maeneo mengine, kwenda kijijini kwake Kilaracha, Moshi Vijijini, Kilimanjaro kwa ajili ya kukutana na "kumaliza matatizo yao."

Mrema, aliyezaliwa siku ya mwisho wa mwaka 1944, alikuwa akisema anampenda sana mama yake, akaanza utaratibu wa kukutana na wanawake wanaoteswa ndani ya ndoa na wanaume wao ili kuwasaidia. Wanawake wakapata mkombozi – wakampenda mno.

Mrema akaimbwa na wanamuziki kwa sifa ya utendaji wake. Remmy Ongala, ghalasa la wanamuziki, akatunga mimbo maalum kwa ajili yake – akiuita Mrema kwa kuwa "alikonga" nyoyo za wanyonge.

Baadaye akaona anaukaribia ukuu zaidi- kuwa kiongozi wa nchi, akaanza vituko vya kiutendaji. Akakwaruzana na wakubwa wake wa kazi. Akafutwa ndani ya CCM, chama alichoapa kukifia. Akaingia upinzani, akagombea urais na kushindwa mara mbili.

Katika harakati zake za kuongoza Tanzania, akageuka ngoma ya askari polisi - aliokuwa kiranja wao – akiamuru wacharaze wapinzani, wakamgeukia yeye kwa kuwa aliingia upinzani.

Mrema, mwana wa Kilaracha – aliyeiaga dunia Agosti 21, 2022, itoshe tu kusema kwamba siasa za Tanzania na harakati za vyama vingi, haviwezi kuandikwa bila kutajwa.

***Sasa ameondoka katika uso wa dunia hii, alale salama.***

# Aquinas: Muumini wa maadili asilia

**Na Deusdedith Kahangwa**

THOMAS Aquinas, alikuwa mwanatheolojia, mwanafalsafa na aliitwa mwalimu mkuu wa Ukristo. Alizaliwa kwenye karne ya 13, katika mji wa Lazio nchini Italia. Baadaye alikuwa kasisi kupitia Jumuiya ya Wadominikani.

Wadominikani ndio waandaaji na wasambazaji wa Jarida la Kimataifa liitwalo "The Thomist," linalochapishwa nchini Marekani.

Aquinas alitengeneza maandiko mengi, lakini andiko maarufu sana linaitwa "Summa Theologica (1265–74)." Huu ni "Muhtasari wa Theolojia" ya Kikristo.

Mtaguso (mkutano wa juu kabisa wa Katoliki) wa Pili wa Vatikano (1962–65) ulikitangaza kitabu hiki kuwa ni "Mafundisho Yasiyochuja."

Mchango mkubwa wa Aquinas kwenye ulimwengu wa wanazuoni ni hoja yake kuhusu maadili ya theolojia asilia.

Katika eneo hili, Aquinas alifundisha kwamba, kwa msaada wa maarifa, siyo yanayotokana na ufunuo katika misahafu pekee, bali yanayotokana na sifa za usanifu ulioko kwenye kimaumbile asilia hapa ulimwenguni.

Ni kwa maarifa yake, binadamu tunaweza kutumia kanuni za kimantiki kutofautisha kati ya wema na ubaya, haki na dhuluma, ukweli na uwongo.

Ni kutokana na mtazamo huu, nadharia ya maadili asilia – yenye kubeba usasa, kama inavyofundishwa na wanafalsafa kama vile Profesa John Finnis wa Uingereza na Profesa Robert George wa Marekani, inajenga hoja kwamba njia asilia ya kukuza ustawi wa binadamu ni kupalilia mema kwa kila binadamu.

Kwa mujibu wa Aquinas, mema kwa binadamu ni pamoja na uhai, chakula, afya, utajiri, maarifa ya kweli, uhuru, haki na urafiki.

Hii maana yake ni kwamba mauaji, njaa, magonjwa, ufukara, ujinga, utumwa, dhuluma, na uadui ni maovu kwa binadamu.



*Thomas Aquinas*

Lakini, kusudi jambo hili liwezekane, inatupasa kuwanoa kifikra watoto wa Tanzania. Katika picha kubwa, tunahitaji kuwafundisha mambo matatu.

Kwanza, kuna falsafa ya ufafanuzi, yaani "descriptive philosophy," kama vile metafizikia, epistemolojia na mantiki. Pili, kuna falsafa ya majukumu, yaani "normative philosophy," kama vile aksiolojia na falsafa ya kanuni za maadili.

Na tatu kuna falsafa matumizi, yaani "applied philosophy," kama vile falsafa ya elimu, falsafa ya utabibu, falsafa ya ujinsia, falsafa ya uchumi, falsafa ya tekinolojia, falsafa ya siasa, falsafa ya dini, falsafa ya uchawi, na kadhalika.

Falsafa ya ufafanuzi ni maarifa ya daraja la kwanza. Falsafa ya majukumu ni maarifa ya daraja la pili, kwani yanategemea maarifa ya daraja la kwanza.

Na falsafa matumizi ni maarifa ya daraja la tatu, kwani yanategemea maarifa ya daraja la kwanza na daraja la pili. Aquinas alikuwa mahiri katika madaraja yote matatu. Tumwige kuanzia leo.

# Askari Pakistan kupelekwa Qatar




PAKISTAN imeridhia kupeleka askari wake kusimamia usalama nchini Qatar wakati wa michuano ya Kombe la Soka la Dunia.

Taarifa iliyotolewa hivi karibuni na Pakistan inaeleza kuwa nchi hizo zilifikia makubaliano hayo kwa lengo la kuimarisha hali ya usalama wakati wa michuano hiyo inayoanza Novemba 21 hadi Desemba18.

Baraza la Mawaziri la Pakistan lilipitisha kwa kauli moja maombi hayo na kwamba nchi hizo zitasaini mkataba hivi karibuni ili askari watakaochaguliwa kwenda Qatar kuanza maandalizi.

Waziri wa Habari na Mawasiliano wa Pakistan, Marriyum Aurangzeb alisema makubaliano hayo yanaonyesha namna nchi hizo mbili zinavyoendelea kuimarisha uhusiano wao kwa faidia ya wananchi wa nchi hizo.

Alisema, kufuatia kuidhinishwa na bunge, sasa majukumu makubwa ya nini askari wa Pakistan watafanya, yataainishwa katika mkataba.

"Makubaliano yanalenga kufafanua majukumu ya pande hizo mbili, taaluma maalum, na idadi ya wafanyakazi wa usalama watakaotumwa kushiriki katika shughuli za ulinzi na usalama," aliongeza.

Wiki iliyopita, Waziri Mkuu wa Pakistan, Shehbaz Sharif alianza ziara nchini Qatar kwa lengo la kukuza ushirikiano na ilielezwa kwamba akiwa huko atapata fursa ya kutembelea makazi ya muda ya askari wa nchi yake watakaokuwepo huko.

Sharif pia ameratibiwa kuzuru uwanja wa soka mjini Doha, ambapo atafahamishwa kuhusu juhudi zilizofanywa na serikali ya Qatar katika Kombe la Dunia.

Katika ziara hiyo, Sharif aliambatana na baadhi ya mawaziri, akiwamo Marryum.

Michuano hiyo ya kombe la dunia ndiyo inatajwa kuwa na idadi kubwa ya watu wanaoifuatilia moja kwa moja, kupitia vyombo vya habari na hata wale wanaohudhuria viwanjani.

Hata hivyo, haijafahamika mara moja muda watakaokuwepo huko wala idadi ya askari hao kutoka Pakistan watakaowasili Qatar.

Kamati maalum ya michuano hiyo inayohusika na masuala ya usalama, nayo haikuwa tayari kueleza idadi ya askari walioombwa kutoka Pakistan.

***Reuters***

# PICHA KUBWA



*Kilele cha mlima mrefu zaidi Afrika, Kilimanjaro ulioko Tanzania, kinaonekana kufunikwa kwa wingi wa barafu. Hali hii imekuwa nadra sana kuonekana baada ya kuelezwa na wataalamu kwamba ongezeko la joto huyeyusha barafu hiyo na mlima kuonekana 'uchi.' Picha hii imepigwa wiki iliyopita na Abdulsamad Abdulrahim.*

*GAZETI hili huandaliwa na kusambazwa na Chama cha Waandishi na Habari Tanzania (Tampa). Pambazuko limesajiliwa na Serikali ya Tanzania, kupitia Idara ya Habari (MAELEZO) na kupewa leseni namba - 00000448.*

TAMPA
TANZANIA MEDIA PRACTITIONERS ASSOCIATION